

## UMOJA WA INJILI

### A KUTAFUTA UMOJA. Wagalatia 2:1-3; Matendo 15.

- ❖ Wafuasi wa dini ya Kiyahudi walipofika Antiokia walisababisha kutokuelewana dhidi ya Paulo na Barnaba.
- ❖ Kisha Mungu alifunua kwao kwamba Paulo, Barnaba pamoja na baadhi ya waamuni Wamataifa walipaswa kusafiri kwenda Yerusalemi kushughulikia mjadala huo pamoja na mitumu na wazee.
- ❖ Mwanzoni mkutano ulikuwa wa siri. Hata hivyo, baadhi ya Mafirisayo wa dini ya Kiyahudi walianza mabishano ya hadhara.
- ❖ Baada ya mjadala mrefu, Kanisa lilikubaliana na Paulo na umoja ulirejeshwa kwa muda kitambo.

### B NDUGU WA UONGO. Wagalatia 2:4-5.

- ❖ Tohara ya nje ilipaswa kuwa mfano wa tohara ya moyo (Kumn. 10:16, 30:6, Yer. 4:4, Warum. 2:29). Inaashiria kuvua kujiamini kwetu na kumtegemea kwa uaminifu Mungu.
- ❖ Kufanya jadi yoyote kuwa sharti la wokovu nikuinyima nguvu ya ukombozi kafara ya Kristo.
- ❖ Hakuna tunaloweza kufanya kuupata wokovu. Wokovu ni zawadi ya bure kutoka kwa Yesu.

### C UMOJA KATIKA UTOFAUTI. Wagalatia 2:6-10.

- ❖ Wayahudi walikuwa na msingi imara wa kibiblia, hivyo wangemkubali Yesu kama Masihi kwasababu alitimiza yote yaliyofunuliwa katika Neno. Utume huo ulikabidhiwa kwa Petro.
- ❖ Paulo alikuwa amejiandaa kuwafikia wale ambao hawakujua ukweli hapo mwanzo. Utume kwa Mataifa ulikabidhiwa kwake.
- ❖ Paulo, Petro na mitume wengine walitumia mbinu tofauti, ila ujumbe ulifanana.

### D KEMEO ANTIOKIA. Wagalatia 2:11-13.

- ❖ Mungu alimuonesha Petro njozi, kisha Petro akaacha kuwachukulia Mataifa kuwa najisi akaanza kuchangamana nao (Matendo 10). Ndio maana Petro aliishi na Wamataifa kwa ujasiri alipotembelea Kanisa kule Antiokia.
- ❖ Hata hivyo, pale baadhi ya Wayahudi walipokuja kutoka Yerusalemi, aliacha kuchangamana na Wamataifa ili awapendeze hao Wayahudi. Mwelekeo wake wakinafiki ulikuwa na mvuto kwa Wayahudi wengine Kanisani.

### E FACING THE CONFRONTATION. Wagalatia 2:14.

- ❖ Petro kula pamoja na Wayahudi kutoka Yerusalemi haikuwa hoja ya msingi, bali kwamba alikuwa anajiweka mbali na Wamataifa kwa maksudi na kutokuwaruhusu kula pamoja na Wayahudi.
- ❖ Matendo yake yakaibua swali, je Wamataifa walikuwa Wakristo wa daraja la pili?
- ❖ Wengi wa Mataifa walifikiri kwamba wangekuwa Wayahudi ili wawe Wakristo(wakikubali fundisho la ndugu wa uongo).
- ❖ Kemeo la Paulo lilikuwa la wazi na lalazima . Jibu la Petro halikuandikwa katika Biblia, ila ni dhahiri alikubali wito wa Paulo na akabadilisha mwelekeo wake.
- ❖ Umoja wa Kanisa na Injili vikashinda.